Jina ..... **Namba yako** .....

102/2
KISWAHILI
Karatasi 2
Oktoba 2016
Muda: Saa 2½

Sahihi ya Mtahiniwa .....

Tarehe .....

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI NDOGO YA KANDARA
KIDATO CHA TATU

KISWAHILI
Karatasi 2
Oktoba 2016
Muda: Saa 2½

www.Manyamfanise.Com

MAAGIZO

a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi iliyoachwa.
b) Jibu maswali **yote**.
c) Andika majibu yako yote katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Alama	Tuzo
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	**80**	

1. SEHEMU A : UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Miongoni mwa haki anazodai mwanamke ni haki ya kutambuliwa kama binadamu mwenye hisi zake. Anataka pia awe na haki ya kurithi mali. Isiwe kazi yake ni kutafuta mali tu, lakini pia apewe haki ya kurithi kwa sababu anachangia pakubwa katika kuyatafuta mali. Jambo hili litasaidia pakubwa maana wanawake ambao hawajazaa wavulana hujipata matatani huku wakishutumiwa kwa sababu ya 'kutoleta mrithi.'

Mwanamke kadhalika anatumiwa vibaya na mwanamume. Yeye ametumiwa kama chombo. Wanamuziki huwa wana makundi ya wanawake ambao kazi yao ni kunengua viuno. Mtu anashangaa ni kwa n ini iwe hii ni kazi ya wanawake ilhali hata wanaume wana viuno. Lengo la wanamziki hawa bila shaka ni kuvutia watu wengi. Wanaume wengi hufika kwa maonyesho ya muziki ili kuwaona wanawake hawa na wala sio kwa sababu ya muziki.

Mikahawa yetu pia ina wasichana ambao huajiriwa kwa kazi kama hii ya kudemka na kunengua viuno ili kuwafurahisha hasa wateja wanaume. Ukweli ni kuwa baa au mkahawa usio na wasichana huwa haupati wateja wengi. Jinsi wanavyodemka hushitua. Lengo hapa sio kuvutia tu lakini pia kutoa pendekezo kuwa "ikiwa una haja nione baada ya kazi."Ajabu ni kuwa wasichana hawa huvaa mavazi haba sana. Amini usiamini warembo hawa wakilinganishwa na wanaume wenzao, kuna tofauti kubwa sana kimavazi. Wanaume huvaa vizuri na kwa hakika hupendeza sana.

Mashindano ya urembo ni jambo lingine ambali linonyesha kuwa mwanamke ananyanyaswa. Anapotembea kwa pozi mbele ya waamuzi ambao ni wanaume anamaanisha nini ? Tena ni nani aliyesema kuwa mwanamke mrembo ni yule mwenye kiuno cha nyigu na miguu ya korongo ? Fikiria kumlazimisha mwanamke kuvaa nguo za kuogelea na kumsimamisha mbele ya umati eti "unaona" urembo wake. Hii ni dhuluma! Mwanamke mrembo kwa maoni yangu sio yule ambaye amenyimwa chakula na kubaki mifupa mitupu! Watembelee wanawake wa kiafrika uone urembo kamili.

Endapo kampuni fulani ina bidhaa mpya za kutangaza, basi hawawezi kufanya hivyo pasi na mwanamke mrembo. Haijalishi iwapo ni simu ya mkono inatangazwa, gari, friji, nguo na vinginevyo. Ni lazima mwanamke awepo. Kwa nini watu wawatumie wanawake kutangaza bidhaa zao na wala sio wanaume ?

Mbona urembo wa mwanamke ulinganishwe na urembo wa gari ? Labda hii ndiyo sababu ambayo imewapelekea wanaume wengi kuwahesabu wanawake miongoni mwa utajiri wao. Yaani miongoni mwa vitu ambavyo mwanamume amemiliki, kuna mwanamke. Picha za warembo wetu zimejaa kwa mabango katika barabara kuu. Ifahamike kuwa binadamu hawezi kulinganishwa na bidhaa na kufanya hivyo ni kumdhulumu.

Isitoshe, kwenye maduka ya uuzaji bidhaa utawapata wasichana wengi kuliko wanaume. Wanawake hawa hutumika kama chombo. Kulingana na mfanyabiashara mmoja mjini, wasichana hasa wale warembo huhuisha biashara. Hivyo hata kabla ya kumwajiri, ni vyema kuangalia urembo na were wake. "Msichana wa kupendeka atatia ladha katika biashara na watu watakuja kununua sio kwa sababu ya mwenye biashara lakini kwa sababu ya muuzaji," anasema mfanyabiashara huyu.

Hata hivyo, mwanamke naye anaonekana kutumia uhuru wake vibaya. Hajilindi na kujiheshimu na labda hii ndiyo sababu mwanamume anaendelea kumnyanyasa. Amejitoa kwa mwanamume ili anyanyaswe na adunishwe. Visa vya wanawake kuteswa na mabwana zao eti kwa sababu hawana kwa kwenda ni vingi. Wengine wanachapwa kila uchao na wanavumilia eti kwa sababu wana watoto. Yaani wanawaona watoto kama kamba au pingu ambazo zimewafunganisha na mabwana zao. Hasa kwa wale ambao walifunga ndoa kanisani sio rahisi kwao kuwataliki wenzao.

Hapo nchini Kenya, inchukuliwa kuwa Koinange ni ya wanawake. Visa vya wanawake kukamatwa hapa ni vingi ajabu ni kuwa wanaume wanaoenda kuwachukua wasichana hawa hawanaswi. Wanawake wengi wamepelekwa mahakamani eti kwa kufanya umalaya lakini wanaume hawaulizwi. Ikumbukwe kuwa huchukua viganja viwili kofi kulia. Hivyo si haki kumdhulumu mwanamke kwa kigezo hicho cha umalaya na kumwacha mwanamume.

Visa vya wanawake kuchukuliwa kwa nia hii ya umalaya na baadaye kutolipwa au wakati mwingine kuchapwa na kuumizwa ni vingi. Itakumbukwa kuwa miaka kadhaa iliyopita mwanamke mmoja alienda kudai malipo baada ya kazi na badala ya kusikilizwa, mwanamke yule aliaibishwa na wanaume alipowapata pale.

Jamii inampamba mwanamke kuwa malaya na kusahau kuwa mwanamke pekee yake hawezi kuwa malaya. Kadhalika, kuna wanaume wengi sana ambao pia huuza miili yao lakini yao hayasemwi. Ajabu gani. Hawakamatwi na biashara zao wanaziendesha vizuri. Hata hivyo, sitoi shinikizo wanawakek waruhusiwe kufanya umalaya lakini nasema kuwa wanawake wasidhulumiwe, watendewe haki.

Maswali

a) Taja namna ambavyo mwanamke anatumiwa vibaya na mwanamume. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

b) Eleza jinsi mwanamke anautumia uhuru wake vibaya. (alama 2)

.....

.....

.....

.....

c) Kwa nini wanawake warembo waajiriwe katika mikahawa na biashara nyingine. (alama 2)

.....

.....

.....

d) Eleza maoni ya mwandishi kuhusu urembo wa mwanamke. (alama 1)

.....

.....

e) Eleza jinsi sheria inavyowabagua wanawake. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

i) kumnyanyasa

.....

ii) wakishutumiwa

.....

iii)shinikizo

.....

www.Manyamfranchise.com

2. SEHEMU B : MUHTASARI
Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali uliyopewa.

Hapa nchini Kenya ukimwi umetangazwa kuwa janga la kitaifa. Hii ni kwa sababu ugonjwa huu umeletea nchi hii maafa yasiyo kifani.

Vifo vingi vimesababishwa na ugonjwa huu. Hapo awali ni vijana waliokuwa wakifa sana lakini katika siku za hivi karibuni, watu wa makamo ndio ambao wameathiriwa sana. Vifo hivi huipokonya nchi hii wafanyakazi na vilevile huiletea nchi ukiwa.

Pia, ugonjwa wa ukimwi unasababisha uyatima. Watoto wengi wameachwa bila wazazi. Hivyo wengi wao wamelazimika kuacha shule ili wawashughulikie wenzao. Kwa kufanya hivyo, watoto hawa wanaingizwa katika majukumu yasiyo yao kwa mfano kutafuta riziki, kulipa kodi n.k.

Serikali nayo inajipata ikitumia kiasi kikubwa cha pesa kwa dawa ya kupunguza makali ya ugonjwa huu maarufu kama ARVs. Kiasi hiki cha pesa kingetumika kwingineko kwa mfano kulipa mishahara au kupanua barabara. Isisahaulike kuwa serikali tayari ina mzigo mkubwa sana wa madeni. Pia akina babu na akina nyanya wamejipata wakiwalea wajukuu wao. Kumbuka waliwalea watoto wao lakini tena wamejipata wakiwalea wajukuu wao. Wazee hawa wanatatizika sana maana hawaelewi njia za kisasa za ulezi. Wengine hata hawana namna.

Kadhalika, ugonjwa huu umeendeleza umaskini kwa watu binafsi na vilevile kwa taifa zima. Kiasi kikubwa cha pesa za mgonjwa au za aila yake huenda kugharamia matibabu ya mgonjwa huyu. Wengine hata hushindwa kuwasomesha watoto maana mzigo wa kununua dawa tayari umewalemea. Hali yao ya kifedha hushuka na kuwaacha maskini wa sina sinani.

Kiwango cha elimu pia kimedidimia maana watoto wengine kwa mfano wale mayatima wa ugonjwa huu hushindwa kumakinika masomoni. Serikali nayo hujipata ikielekeza kiasi kikubwa cha fedha kwa ununuzi wa madawa na kwa kuwaelimisha raia wake kuhusu ugonjwa huu. Pesa hizi pengine zingelipa mishahara au kununua vitabu.

Watoto wachanga kwa mfano, wale walio tumboni au wale ambao wamenajisiwa hujipata wameambukizwa ugonjwa huu. Matokeo yake ni kupata idadi ya watu iliyo na wagonjwa wengi ambao hawawezi kuzalisha mali. Malezi ya watoto walioambukizwa huwa magumu na jamii kwa jumla hukosa amani na furaha kwani huishi kwa mahangaiko.

Mashirika mengi ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yamebuniwa eti kuwasaidia waathiriwa wa ugonjwa huu. Mengine ni mazuri na mengine yamejaa unafiki na hivyo kupalilia ufisadi. Baadhi ya mashirika huchukua fursa hii kuomba misaada kutoka nchi za ng'ambo. Misaada hii mara nyingi haiwafikii walengwa na huishia mifukoni mwa wakurugenzi wa mashirika haya. Kuna watu wengi ambao wametajirika kutokana na ulaghai huu.

Magonjwa mengine ambayo yalikuwa yakizuka kwa nadra sana sasa yamekuwa jambo la kawaida. Magonjwa haya ni kama vile utando wa ubongo, homa ya mapafu, kifua kikuu n.k. Yamekuwa ya kuwaua watu kinyume na zamani ambapo hata hayakuwa yakisikika.

Hata hivyo, tusikate tamaa kwa sababu ya ugonjwa huu. Tujaribu sana kuepuka tabia ambazo zinaueneza ugonjwa huu kama vile ukahaba na nyinginezo. Huko hospitalini wahudumu wawe waangalifu ili watoto wanaozaliwa na wazazi wenye virusi wasiambukizwe.

Kadhalika, serikali nayo itafute njia za kuwasaidia waathiriwa kupata dawa za kupunguza makali ya Ukimwi. Pana haja pia ya kuwaelimisha Wakenya kuhusu madhara na athari za ugonjwa huu kwa kina ili wajiepushe na vitendo vinavyowahatarisha. Makundi ya waathiriwa yaundwe ili waweze kupata namna ya kusaidiwa. Kwa mfano, wanaweza kupewa mikopo ya kuanzisha biashara ili wajikimu.

Ukimwi usipochungwa utawafyeka Wakenya na kuliacha taifa pasi na wafanyakazi au watu wa kuliendeleza. Hivyo ni vyema kutambua kuwa kwa hakika ugonjwa huu ni janga la kitaifa ili hatua za dharura zichukuliwe.

a) Kwa nini ukimwi ni janga la kitaifa. (Maneno 70) (alama 9)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

www.Mang'u-franchise.com

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b) Mwandishi anatoa pendekezo gani kuhusu hali hii. (Maneno 40) (alama 6)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika kwa umoja. (alama 2)

Someni wanetu, msicheze na dunia. Mnasikia ?

.....

www.Manyamfranchise.com

b) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo : (alama 1)
Kijakazi aliangika vyombo vya tajiri wake.

.....

.....

.....

.....

c) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Juma alimlimia mama shamba kwa jembe.

.....

d) Tumia neno 'vizuri' kama : (alama 2)
i) Kivumishi

.....

ii) Kielezi

.....

e) Onyesha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi hii: (alama 2)
Mgeni aliyekuja shuleni jana alikaribishwa kwa furaha.

.....

.....

f) Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi hii: (alama 2)
Alipofika alimwona pale alipokuwa amelala.

.....

.....

g) Andika katika hali timilifu
Wazee wa kijiji watakata kesi hii.

.....

h) Kanusha sentensi hii : (alama 2)

Ukilala sana utapona haraka

.....

.....

i) Ainisha vitenzi katika sentensi hizi : (alama 2)

i) Juma ni mchezaji stadi.

.....

www.kanyanfranchise.com

ii) Hamisi alikuwa mgonjwa jana asubuhi

.....

j) Sahihisha sentensi hii : (alama 1)

Ningekuwa mwanafunzi ningalisoma kwa bidii

.....

.....

k) Ainisha mofimu : (alama 1)
Alimlia

.....

l) Andika katika hali ya udogo. (alama 2)

Ng'ombe wangu ana ndama mkubwa.

.....

m) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi : (alama 2)

i) andika

.....

ii) shona

.....

n) Weka nomino hizi katika ngeli zake. (alama 2)

i) kiboko

.....

ii) maziwa

.....

o) Andika katika usemi wa taarifa : (alama 3)
"Nimekuwa nikija kwenu kila siku lakini nimeamua kulikata guu langu." Hamisi alimwambia Rehema.

.....

.....

p) Konsonanti hizi hutamkiwa wapi ? (alama 2)

i) / n /

.....

ii) / p /

.....

www.Maayamfranchise.Com

q) Changanua kwa matawi. (alama 4)
Mama na mtoto wake wanalima vizuri

.....

.....

.....

.....

.....

r) Andika upya kwa kutumia 'O' rejeshi. (alama 1)

Mchezaji ambaye alicheza vizuri alituzwa.

.....

s) Unganisha ili kuonyesha hali ya kuamrisha. (alama 1)

Wewe + sije

.....

t) Ainisha viambishi. (alama 2)

Alichezesha

.....

4. ISIMUJAMII

A. Unanuia kufanya yepi sasa ?

B. Nitampeleka kwa theatre kesho asubuhi ili nikate huo uvimbe kisha nitampa natibiotics.

a) Hii ni sajili gani ? (alama 2)

.....

b) Eleza sifa nne za sajili hiyo. (alama 8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Www.Manyanifranchise.Com